



United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

Kuwapatia Vijana Huduma za Ujinsia na Afya ya Uzazi:

Mwongozo kwa Watoa huduma za Afya


Je, Ulijua?

- ✗ Vijana 52 kati ya milioni 158 wa nchi za mashariki na kusini mwa Afrika, hupata maambukizo ya VVU kila saa.
- ✗ Katika baadhi ya nchi, Maambukizo ya VVU ni sababu inayoongoza kwa vifo vya vijana.
- ✗ Msichana mmoja kati ya watano hupata mimba akiwa na umri wa miaka 17.
- ✗ Mimba na kujifungua ni kisababishi cha pili kikubwa cha vifo vya wasichana wenye umri wa miaka 15-19 duniani kote.
- ✗ Vijana walio wengi wanakosa taarifa sahihi kuhusu ujinsia na afya yao ya uzazi.

Ili kuwa na afya nzuri ya ujinsia na uzazi, vijana wanahitaji maarifa, uwezo na huduma za kufanya uamuzi chanya, wenye taarifa za kutosha, salama na uwajibikaji unaohusu ngono na ujinsia.

Hii ni haki yao.

Baadhi ya vikwazo vya mawasiliano vinazuia watoa huduma kutoa huduma za ngono na afya ya uzazi kwa vijana. Kipeperushi hiki kinajumuisha mapendekezo ya kusaidia kukabiliana na vikwazo hivyo na kuwasaidia vijana kikamilifu.



**Youth Friendly
SRH Services:
It Starts with YOU!**

KIKWAZO

Maarifa



“Sijui vya kutosha jinsi ya kuelezea hili kwa kijana”

Mtazamo



“Kijana huyu hapaswi kuzungumza kuhusu ngono”

Tofauti za Kijamii na Kiuchumi



“Nitazungumzaje na kijana kuhusu SRH wakati mimi ni mtu mzima sana/ wakati hatuna utamaduni/ dini moja; tuna jinsia tofauti, au yeye ni tajiri sana/ maskini sana kuliko mimi”

Lugha



“Kijana hawezi kuelewa dhana za kitibabu ninazozitumia”

Muda



“Nina kazi nyingi sina muda wa kuzungumza na vijana kuhusu SRH”

Mahali



“Chumba hiki kina kelele sana / hakina utulivu wa kufanya mazungumzo yetu”

UWE CHACHU YA MABADILIKO

Nenda na wakati. Kama hujui jambo fulani, mwambie kijana kwamba utamtafutia, chukua mawasiliano yake na kisha fuatilia.

Uwe mkarimu. Wajibu wako ni kutoa huduma za afya kwa wale wanaozihitaji, sio kuhukumu au kuanzisha maoni yako dhidi yao.

Unaweza kuwa tofauti na mtu anayehitaji huduma zako, lakini wajibu wako ni kuhakikisha afya.

Wafanye wajisikie vizuri; usiwahukumu na tambua na kujali wasiwasi walio nao. Heshimu maadili yao, hata kama hukubaliani nayo.

Rahisisha lugha yako na hakikisha wameelewa kile mlichoshirikishana. Kama sio, fafaua dhana au tumia maneno rahisi.

Tenga muda hususan kwa vijana kuja kwako kwa ajili ya kupata huduma – kumbuka ratiba zao. Mlenge kijana unayezungumza naye, usionyeshwe kukata tamaa au kuwa na kazi nyingi kwani hili linaweza kuleta ugumu katika kuwasiliana vizuri.

Fanya chumba kiwe kizuri na chenye mvuto kwa vijana. Hakikisha ni rahisi kuingia na vijana wanaweza kukutembelea kwa usalama, bila kuwa na hofu kwamba wataonekana.

Ujana balehe ni kipindi cha mabadiliko makubwa ya kimwili, kitabia na kihisia.

Ili kufanya uamuzi wakiwa na taarifa za kutosha kuhusu afya yao ya kingono, vijana wanahitaji taarifa kuhusu mabadiliko haya na kuhusu ujinsia.

Kuhakikisha ujinsia na afya ya uzazi ni kuhusu maarifa, ujuzi na kupatikana kwa huduma ya afya; NA kuhusu kuwa na uwezo wa kufanya uamuzi mzuri, wenye taarifa ya kutosha, salama na wenye wajibu kuhusu ngono na ujinsia.

Taarifa inasaidia vijana kuchelewa kuanza vitendo vya ngono; lakini wanahitaji pia kupata kingamimba, wakati wanapoamua kufanya ngono.

Elimu ya kina ya ujinsia inahusu kuwapatia taarifa kulingana na umri kuhusu ngono salama na afya bora ya uzazi na ukuaji, inajumuisha mada kuhusiana na: uhusiano, maadili, mtazamo na stadi; utamaduni, jamii na haki za binadamu; ukuaji wa binadamu; mwenendo wa kingono na afya ya ujinsia na uzazi.

Watoa huduma wanahitaji kuhakikisha kwamba vijana wanapata maarifa na huduma wanazozihitaji ili kufanya uamuzi unaofaa na kujilinda wao wenyewe na wengine dhidi ya madhara yasiyokusudiwa ya ngono, ikiwa ni pamoja na kupata Maambukizo kwa Ngono (STI), VVU na mimba zisizotarajiwa.

Kiwango cha chini cha Huduma

Watoa huduma wanapaswa kujiandaa kuwapa ushauri vijana kuhusu:

- ✘ Balehe, viungo vya uzazi; ngono; mzunguko wa maisha ya kingono; mwenendo wa kingono na mwitiko wa kingono; na ujinsia.
- ✘ Uzuiaji wa mimba, ikiwa ni pamoja na utoaji wa kingamimba na kingamimba za dharura.
- ✘ Kuelewa, kutambua na kupunguza uwezekano wa maambukizo kwa ngono na VVU, ikiwa ni pamoja na dawa za kuzuia VVU kuzaliana mwilini (post-exposure prophylaxis) kwa ajili ya kuzuia ueneaji wa VVU.

Ofisi ya Kanda ya SAfAIDS, Zimbabwe:

Barabara ya 17 Beveridge, Avondale, S.L.P A509, Avondale, Harare, Zimbabwe

Simu: +263 4 336 193/4, Faksi: +263 4 336 195

Tovuti: www.saf aids.net

